BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWAMWAKA WA FEDHA 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kutumia fursa hii adhimu kwa kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala, Mwingi wa Rehma na Mwenye Kurehemu, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kila siku kwa hali ya usalama na amani.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii mbele ya Baraza lako Tukufu. Ripoti ambayo inaonesha shughuli zetu zote ambazo tumezitekeleza kuanzia mwezi wa nane 2023 mpaka Mwezi wa Pili 2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na Kanuni 107(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020).

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kutumia nafasi hii tena kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati yetu kufanyakazi zake kwa ufanisi na uweledi zaidi. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo: -

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdalla Hussein Kombo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 9. | Nd. Talib Enzi Talib | Katibu |
| 10. | Nd. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| 11. | Nd. Bakar Makame Haji | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utaratibu uliowekwa katika kazi za Kamati kwa muda wote uliopita, Kamati yetu ilipanga kufuatilia utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara zifuatazo: -

1. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
2. Wizara ya Afya.
3. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.
4. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) baina ya Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba nianze kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati hii ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama inavyoelekezwa na Kanuni 109(15) ya Kanuni za Kudumu za Baraza (Toleo la 2020).

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## PROGRAMU KUU YA ELIMU YA JUU

## CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

**Mheshimiwa Spika,**

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni Chuo Kikuu pekee cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Chuo hiki kilianzishwa chini ya Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999 sambamba na marekebisho ya Sheria ya Chuo, Nam. 11 ya mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,**

katika ufuatiliaji wa Programu hii katika Chuo Kikuu cha Suza, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zinazozikabili skuli mbali mbali katika chuo hiki, ikiwemo changamoto ya msingi ya Uendeshaji wa Mfumo wa pamoja wa vyuo na taasisi zilizo chini ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ambao unadaiwa kulalamikiwa karibu na skuli zote.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kutoa maelekezo kuhusu Mpango mpya wa mageuzi ya Chuo Kikuu cha

SUZA katika uendeshaji wa Taasisi zake ili kuweka sawa mfumo huo na kuweza kukubalika na kutumika katika vyuo na skuli husika.

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto nyengine inayokabili katika chuo cha SUZA ni uwepo wa mishahara midogo katika Chuo Kikuu hicho ukulinganisha na Vyuo au Taasisi nyengine. Kamati inashauri Serikali licha ya kuwa imeanza kuzingatia kufanya marekebisho ya mishahara katika chuo hicho, bado kuna haja ya kupewa bajeti zaidi ya mishahara ili angalau viwango vya mishahara vitakavyowekwa vilingane ama kukaribia na viwango vya vyuo na taasisi vyengine katika nchi ama maeneo tuliyokaribu nayo.

**Mheshimwa Spika,**

Aidha, Suza inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa majengo na miundo mbinu katika majengo yake hali inayohitaji ukarabati na matengenezo makubwa. Mfano katika Skuli ya Benjamin Mkapa, Kamati ilibaini kuwepo kwa hali hiyo hivyo inashauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu suza, zinatumika vizuri katika ukarabati wa majengo katika kampasi zake zote zinazosimamiwa na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Tawi la chuo cha Teknologia cha INDIAN MADRAS.  Hatua hiyo itatimiza lengo la Serikali la kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo cha Vyuo vikuu Bora. Hata hivyo Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara kuweka mazingira mazuri ili chuo kufikia malengo na dhamira ilokusudiwa.

BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR.

**Mheshimiwa Spika,**

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni miongoni mwa taasisi za elimu ya juu na majukumu yake ni pamoja na kutoa mikopo ya kugharamia elimu ya juu kwa wanafunzi**,** Kufuatilia marejesho ya mikopo hiyo kwa wahitimu na Kutafuta nafasi ya ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa katika Chombo hiki; zikiwemo kuchelewa kupatikana kwa fedha za mikopo ili kuweza kuwalipa mapema wanafunzi vyuo vinapofunguliwa, Utafutaji wa vyanzo vipya vya mapato ya Bodi baada ya kodi ya Skill Develepment Levy kuondolewa na SMZ**,** Kupatikana kwa jengo la kudumu la Bodi Unguja na Pemba**,** Ongezeko la wanafunzi wanaohitaji kusoma nje ya nchi pamoja na Kupatikana kwa Gawio la fedha za Mikopo kutoka SMT /HESLB kwa ajili ya Zanzibar.

**Mheshimwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya fedha na Mipango kuhakikisha kuwa inawaingizia fedha mapema Bodi ya Mikopo ili iweze kuwalipa wanafunzi kwa wakati.

**Mheshimwa Spika,**

Kuhusu suala la Kupatikana kwa Gawio la fedha za Mikopo kutoka SMT ama HESLB kwa ajili ya Zanzibar, Kamati inaishauri serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais kulifatilia suala hili kwa vile Kamati imebaini kuwa ni suala la kisera zaidi ambapo mazingatio na utekelezaji wake unahitaji mazungumzo kati ya Serikali ya SMZ na SMT. Kamati imebaini kuwa iwapo Zanzibar itapatiwa gawio hilo la fedha la asilimia 10 ya Bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania Bara (HESLB) itaweza kupata zaidi TZS Bilioni 70 ambazo zitakidhi haja katika kutoa mikopo ya kugharamia elimu ya juu kwa wanafunzi wa Zanzibar.

**Mheshimwa Spika,**

Kamati inapongeza Wizara kwa kutunga Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu Zanzibar. Kamati imebaini kuwa uwepo kwa Sheria Mpya kutasaidia kurekebisha changamoto mbali mbali zikiwemo kuwapatia mikopo Wanafunzi kwenye ngazi ya Stashahada na Astashahada.

Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza BAJETI ya Mikopo ya wanafunzi kutoka Tanzania shilingi 19.50 Bilioni kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia Tanzania shilingi 29.05 Bilioni katika mwaka wa fedha 2023/2024.

## PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI

**Mheshimwa Spika,**

Kamati katika ufuatiliaji utekelezaji wa Programu hii, imeweza kutembelea sehemu mbali mbali ili kufahamu changamoto na mafanikio na kuweza kuishauri Serikali.

## SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI YA MIKUNGUNI

Miongoni mwa changamoto inazozikabikli Skuli hii ni pamoja na Uchakavu wa majengo ya skuli na hali ya mazingira isiyoridhisha, Uhaba na uchakavu wa Mashine ambazo zimeonekana kuharibika mara kwa mara, Uchakavu wa Dakhalia ya wanafunzi wa kiume na wakike, hali inayosababisha wanafunzi kuishi katika mazingira magumu ya kimasomo na Ukosefu wa usafiri kwa wanafunzi, hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu wakati wanafunzi wanapohitaji kwenda kufanya mafunzo ya kujifunza katika Taasisi tofauti za Serikali.

**Mheshimwa Spika,**

Kamati inaishauri wizara kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuzifanyia ukarabati kwa ajili ya kuziimarisha Skuli za Ufundi ya Mikunguni Unguja na ile ya Kengeja Pemba ili uweze kufanyika kwa wakati kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa kuweka utaratibu maalum kwa wanafunzi wanaotoka Skuli hizo ili kuweza kuendelea na masomo yao katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KITS) kwa kuwapunguzia gharama za malipo ya masomo ili nao waweze kuendelea na masomo yao ya sayansi, kwani hivi sasa Zanzibar ina uhaba wa wataalamu wa masuala ya ufundi.

## PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

**Mheshimwa Spika,**

Lengo kuu la Programu hii ni kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa katika ngazi zote za elimu ni yenye ubora kwa manufaa ya jamii na Taifa kwa ujumla.

## TAASISI YA ELIMU

**Mheshimwa Spika,**

Taasisi hii inakabiliwa na changamoto za Uhaba wa watumishi katika idara na vitengo vyake, Ukosefu wa ofisi ya kudumu na yenye nafasi unguja na pemba, Kutokamilika kwa sheria ya taasisi ya elimu na Bajeti ndogo ya taasisi.

Kamati inaipongeza Taasisi kwa ubunifu katika utekelezaji wa kazi zake kwa ufanisi licha ya kuwa inakabiliwa na changamoto ya ufinyu mkubwa wa Bajeti. Aidha, Kamati pia inashauri Wizara kukamilisha mchakato wa kuanzisha Sheria ya Taasisi ya Elimu ili kuweza kutekeleza ipasavyo matumizi ya mtaala mpya.

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kukamilisha mchakato wa uchapishaji wa vitabu vya kufundishia kwa mujibu wa mtaala mpya wa elimu sambamba na mafunzo kwa walimu yanahitaji kuendelezwa ili yaende sambamba na matumizi ya mtaala mpya

## OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR

**Mheshimwa Spika,**

Jukumu kuu la Ofisi hii kufanya ukaguzi wa elimu kwa skuli zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari zilizosajiliwa pamoja na Taasisi zinazotoa Mafunzo ya Ualimu, Vyuo vya Elimu Mbadala, Elimu ya Watu Wazima, Taasisi za Elimu zilizosajiliwa zilizo nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwepo kwa Uchakavu na ufinyu wa nafasi katika jengo la mkaguzi Mkuu wa Elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzingatia kuzipatia ofisi za kudumu Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu pamoja na Ofisi za Wakaguzi wa Elimu Mikoa ili taasisi hiyo iweze kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Aidha, Kamati inapendekeza kwa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2024/2025, suala la upatikanaji wa usafiri wa kudumu kwa Ofisi hiyo ni muhimu kupewa kipaumbele ili taasisi hiyo iweze kusimamia ipasavyo ubora wa elimu katika skuli zetu. Sambamba na Wizara kuharakisha kuunda Baraza la Elimu ili kutoa nguvu za kisheria katika kutoa maamuzi dhidi ya makosa katika sekta ya elimu.

## BARAZA LA MITIHANI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati haikuridhishwa na mazingira ya jengo la ofisi za Baraza la Mitihani kutokana na umuhimu wake. Hali ya jengo ni chakavu sana na haliko katika mazingira rafiki kwa ajili ya matumizi ya ofisi hiyo ambayo ni chimbuko la kutoa wataalamu bora katika nchi.

Aidha, Kamati inaishauri wizara kuzingatia kupatikana kwa mtambo wa kisasa wa uchapishaji wa mitihani ili Baraza liweze kujitegemea kufanya shughuli zake na kuepuka gharama kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kupitia Baraza la Mitihani kwa kusimamia ufanyaji, usahihishaji na Kutoa Matokeo mazuri ya Mitihani ya Darasa la Nne yenye asilimia ya ufaulu 91.35 na asilimia 95.00 kwa ufaulu wa darasa la Saba katika mwaka wa masomo 2023.

## PROGRAMU KUU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kufanya tathmini ili kufahamu muitiko wa maendeleo ya vyuo vyengine vya mafunzo ya amali vilivyopo nchini.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuvizingatia vyuo vya mafunzo ya mali kuwa na muundo maalumu tofauti na taasisi nyengine ili kuwawezesha watendaji wanaostakihi kupata haki zao kwa mujibu wa muundo wa vyuo.

Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ya vyuo vya mafunzo ya amali kutoa wanafunzi ambao wataweza kutoa ushindani katika soko la ajira katika sekta binafsi.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina lengo la kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji na upatikanaji wa elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inatekelezwa ipasavyo Miradi ya Kuimarisha elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi (HEET)na mradi wa kuimarisha ujuzi kwa vijana katika kujipatia ajira katika Uchumi wa Buluu (SEBEP).

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuunda Kamati ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mikataba inayoingiwa baina ya Serikali na Wakandarasi mbali mbali kwa lengo la kujenga usimamizi imara na madhubuti kwa wataalamu wetu wa ndani.

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi kubwa walizochukua katika kufanya ukarabati na ujenzi wa Madarasa na Majengo ya Ghorofa ya kisasa ya Skuli mbali mbali kwa Unguja na Pemba katika kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki na salama. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipunguza mzigo Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara kushughulikia na kusimamia miradi yote ya ujenzi kwa kurudisha Idara ya Ujenzi kama ilivyo kuwa awali kwa lengo la kupunguza changamoto zinazojitokeza za matumizi makubwa ya fedha za ziada (variations) kinyume na utaratibu uliopo kisheria.

Vile vile , Kamati inapongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa ya kutayarisha Rasimu ya Sera mpya ya elimu sambamba na  kazi ya matayarisho ya Mpango wa utekelezaji wa Mageuzi ya Elimu wa miaka saba mpaka 2030 ambayo Rasimu ya Mpango huo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari 2024 na kutumika katika zoezi la matayarisho ya Bajeti ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## WIZARA YA AFYA

## PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri Wizara katika Mpango wa kuviimarisha vituo 74 vya afya kuhakikisha kuwa wataalamu wa afya wanashirikishwa ipasavyo katika Miradi ya Ujenzi wa Vituo hivyo ili kuondokana na changamoto mbali mbali zinazoweza kujitiokeza wakati wa utoaji wa huduma.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha taratibu za manunuzi ili Mpango wa ujenzi wa kuviimarisha vituo vya afya uweze kutekelezwa kwa wakati.

## PROGRAMU KUU YA TIBA

## WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea bajeti Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa kwa lengo la kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi ili kuondokana na uchelewaji wa uangizaji wa dawa nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Serikali Mtandao kurekebisha kasoro ndogo ndogo ambazo zinasababisha kuzorota kwa suala la urahisishaji wa usambazaji wa dawa kupitia Mtandao.

Kamati inaipongera Wizara kwa kuweza kupitisha sheria ya Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwani itakwenda kuimarisha upatikanaji wa

huduma ya dawa na vifaa tiba kwa wananchi.

## MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni wa changamoto ambazo kamati imebaini katika Taasisi ya Mfamasia mkuu wa serikali ni pamoja na kutokuwepo kwa muongozo wa matibabu wa mwaka 2014(Standard Treatment Guidelines). Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kazi ya uchapishwaji wa Muongozo huo. Sambamba na Orodha ya dawa muhimu ya mwaka 2015 ili uweze kusambazwa na kutumika katika hospitali zote na vituo vya afya ndani ya nchi. Kamati imebaini kuwa kutokuwepo kwa muongozo huo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 sasa kunahatarisha utoaji wa huduma za afya kwa jamii nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na jitihada za uimarishaji wa ongezeko la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni ya zamani ya dawa, Kamati inaishauri Wizara kupitia Mfamasia Mkuu wa Serikali kuhakikisha inakamilisha ulipaji wa madeni hayo ili Serikali iweze kuondokana na mzigo huo wa deni.

## WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa jengo jipya la Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodizi pamoja na vifaa vya uchunguzi vilivyowekwa katika jengo hilo kuwa linatuzwa ili kuwa na taasisi ya kitaalamu imara na yenye ubora. Mradi wa Jengo jipya la Maabara ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ni mradi wa Maendeleo wa SMZ uliogharimu jumla ya shilingi bilioni 5.4 na awamu ya pili ni ya ununuzi wa vifaa vya maabara ambao umegharimu jumla ya shilingi Bilioni 4.4.

Aidha, Kamati imeishauri Wizara kuanzisha kituo cha pamoja ONE STOP CENTER katika maeneo ya uingiaji wa bidhaa kama bandari ili kudhibiti uingiaji wa bidhaa zisizokubalika za dawa na chakula pamoja na kurahisisha usimamizi wa mfumo wa biashara na bidhaa hizo ambazo zinaingia kutoka nchi na maeneo tofauti.

## PROGRAMU KUU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kuimarisha huduma za First Track katika hospitali hiyo ili huduma hizo ziweze kufikia kiwango kinachostahili.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuimarisha upatikanaji wa vyanzo vya mapato vitokanavyo na huduma za afya ili sekta ya afya iweze kufanikisha kutoa huduma zenye viwango na ubora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilitembelea katika Hospitali ya Wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu ambayo ipo chini ya Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na kubaini changamoto mbali ikiwemo; kuwepo kwa mnyororo mkubwa wa utoaji wa huduma unaopelekea watendaji katika hospitali hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuangalia namna itakayoweza kuifanya Hospitali ya wagonjwa wa akili kuweza kujitegemea au kuwa na kasma ya Fungu maaulum la matumizi. Kamati imebaini kuwa kuna mnyororo mkubwa wa utoaji wa huduma unaopelekea watendaji katika hospitali hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kutokana na kuchelewa kupata mahitaji ya huduma muhimu za hospitali ambazo huduma hizo mpaka zitolowe kupitia Hospitali ya Mnazi Mmoja.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA URATIBU WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Utekelezaji wa Mradi huo unakuwa na ufanisi na unaanza kwa mujibu wa wakati uliopangwa. Kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa na nia njema ya kutekeleza mradi huo lakini kumejitokeza baadhi ya vikwazo ama changamoto katika utekelezaji huo zikiwemo: kuchelewa kupatiwa fedha za Bajeti za uendeshaji katika kitengo cha usimamizi wa Mradi (PIU) jambo ambalo limesababisha deni kwa mujibu wa makubalinao ya utekelezaji wa mradi. Pia kuna taratibu za kisheria kuhusu matumizi ya mji mkongwe zinazozuia kuvunja baadhi ya majengo ya zamani katika hospitali ya Mnazi mmoja kwa ajili ya matumizi ya Mradi.

Kamati inaishauri Wizara kuwapatia fedha za Bajeti za uendeshaji katika kitengo cha usimamizi wa Mradi (PIU) ili kazi za usimamizi wa mradi huo ziweze kuendelea badala ya kusubiri fedha za Mradi ambazo zimekua na urasimu unaosababisha kuchelewa kwa mradi.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inazifuatilia na kuzisimamia ipasavyo Kampuni Binafsi (outsource) zilizoingia makubaliano ya kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kutoa baadhi ya huduma katika Hospitali za umma ili kuona huduma hizo zinatolewa kwa ubora na ufanisi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kutoa majibu kwa Kampuni za huduma za outsouce wanapowasilisha mahitaji ya huduma zinazohitajika katika Hospitali na vituo vya afya zinazotoa huduma hizo.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

## PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa Programuu hii zikiwemo; uchakavu wa majengo ya muda mrefu ya hifadhi ya wazee, kuwepo kwa utaratibu usioridhisha wa upatikanaji wa Pencheni jamii kwa wazee, kuendelea kuibuka kwa kesi mbali mbali za udhalilishaji wa Watoto na kuwepo kwa utitiri wa nyumba zisizorasmi za kulelea Watoto.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya Wizara kuendelea kufanya matengenezo katika makaazi ya wazee Welezo, Sebleni na Limbani; Kamati inaishauri Wizara kukamilisha mpango wa ukarabati mpya wa makaazi hayo ili wazee hao waweze kuwa na makaazi bora zaidi.

Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wadau wake kubuni mbinu muafaka zitakazoweka uratibu bora zaidi utakaohakikisha kuwa taarifa za wazee watarajiwa zinapatikana na kuingizwa katika mfumo endelevu wa kielektronik,

Kamati imebaini kuwa kuna usumbufu kwenye utowaji wa pencheni jamii hivyo Kamati inaishauri Wizara kuandaa utaratibu nzuri ili kutatua changamoyo hizo.

Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuimarisha huduma katika kuwasaidia watu wenye mazingira magumu zaidi kwa kuwafikia katika maeneo yao husika.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuwasilisha mapendeezo ya wazee ya kutaka kuwepo kwa Jumuiya ya wazee sambamba na uwakilishi wao katika chombo muhimu cha kutunga sheria.

Kamati inaipongeza Wizara kuendelea kuwatunza na kuwahudumia watoto katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini. Sambamba na kuhifadhi misaada mbali mbali ya vifaa na fedha kutoka kwa watu binafsi, taasisi za jamii, na taasisi za Serikali kwa ajili ya kusaidia huduma za kituo hicho. Hata hivyo Kamati imeshauri Wizara kufunguliwa Account ya Benki kwa ajili ya kuhifadhiwa fedha zitokanazo na misaada ya Watoto wanaoishi katika nyumba hiyo.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Progarmu hii , Kamati ilibaini changamoto mbali mbali zikiwemo; kutokamilika kwa mpango kazi mpya wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto (NPA-VAWC 2023-2028), Uwezo mdogo wa vikundi vingi vya wajasiri amali wanawake katika kujiendeleza kiuchumi, Kuhitajika kwa elimu zaidi ya kuhamasisha Jamii kuhusu mapambano dhidi ya udhalilishaji, Utaratibu mzima usioridhisha wa malipo ya pencheni jamii kwa wazee, Kukosekana kwa kanuni katika Sheria ya Wazee na Kufanyiwa mapitio Sheria ya Mtoto .

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kukamilisha kwa wakati uandaaji wa Mpango kazi mpya wa kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ili uweze kusaidia katika kuanzisha juhudi mpya za mapambano dhidi ya udhalilishaji.

Kamati inaipongeza Wizara kwa juhudi zake za kuendelea kuelimisha na kuhamasisha Jamii kuhusu mapambano dhidi ya udhalilishaji.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwakutanisha Wajasiriamali Wanawake ili waweze kuwa na sauti ya pamoja na kuibua changamoto zao na kuziripoti katika ngazi mbali mbali ili kupatiwa ufumbuzi, ikiwemo

changamoto za uhaba wa masoko, mitaji, fursa za elimu ya ujasiriamali na kutunza kumbukumbu za Fedha.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kukamilisha maboresho ya maeneo yenye changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Mtoto pamoja na kuandika rasim ya sheria hiyo ili kuweza kuwa na sheria rasmi ya mtoto.

## WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

## SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini changamoto mbali mbali inazolikabili Shirika hili zikiwemo; Kuwepo kwa Deni kubwa ambalo Shirika linazidai taasisi za Serikali jambo ambalo linazorotesha ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zilizopangwa, Gharama kubwa za uchapishaji wa magazeti kutokana na shirika kutokuwa na mtambo wake wa kuchapishia magazeti na kupelekea shirika kuchapisha magazeti yake kwa kampuni binafsi pamoja na uhaba wa nafasi katika jengo la Shirika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya fedha na mipango iweze kutekeleza maagizo ya kukata deni kwa taasisi zinazodaiwa japo kwa asilimia kwani kamati inatambua kwamba serikali imetoa agizo la kukatwa taasisi zinazodaiwa moja kwa moja kutoka OC zao ili shirika lipate mtaji ili liweze kujiendesha.

Kamati inalipongeza Shirika la Magazeti ya Serikali kwa kufanikiwa kutekeleza shughuli zake kwa kutumia mapato yake ya ndani licha ya Shirika hilo kusitishwa ruzuku kutoka serikalini.

Kamati inaipongeza wizara kupitia Shirika kwa kuchapisha nakala 3,000 za Jarida la Neema Zetu na kuzisambaza bure kwa wananchi kwa lengo la kuwahabarisha juu ya utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya serikali ya awamu ya nane.

## SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA -ZBC

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini changamoto mbali mbali inazozikabili Shirika zikiwemo Uhaba wa wafanyakazi ZBC TV, Uhaba wa vitendea kazi na mitambo ya kisasa kama vile setelight, k
Pemba, Uchakavu wa jengo kongwe Pemba ambalo linahitaji ukarabati mkubwa pamoja na ukamilishaji wa marekebisho ya Sheria Namb.4 ya ZBC ya mwaka 2013 na Kanuni zake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inalipongeza Shirika la ZBC kwa kuwa na mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa kazi zake licha ya kuwa na changamoto mbali mbali inazozikabili shirika hilo.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya China kufanya matengenezo makubwa ya ZBC Redio. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika ukarabati huo ili kituo hicho kiweze kuwa katika hali nzuri na kufanyakazi kwa ufanisi.

Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha marekebisho ya Sheria Namb.4 ya ZBC ya mwaka 2013 pamoja na mapitio ya kanuni. Kuwepo kwa sheria mpya kutaondoa kasoro mbali mbali za kiutendaji zilizomo katika taasisi hiyo.

## MRADI WA UKARABATI WA UWANJA WA AMAANI NA GOMBANI

Mheshimiwa Spika,

Wizara inaendelea na utekelezaji wa Uimarishaji wa miundombinu ya michezo Zanzibar. Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amani Unguja na Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani Pemba imetekelezwa na imefikia katika hatua mbalimbali.

Changamoto za msingi katika miradi hii ambazo Kamati imebaini ni kuchelewa kuingizwa fedha kwa wakati ili kuweza kukamilisha maeneo zaidi ya miradi pamoja na kuongezeka kwa gharama za Bajeti za awali.

Mheshimiwa Spika,

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha viwanja vipya vya AMANI COMPLEX vinatuzwa na kuenziwa ili kuweza kutumika katika shughuli za michezo ya kitaifa na kimataifa.

Kamati inaishauri wizara ya fedha kuingiza fedha za miradi kwa wakati ili ipate kumaliza kwa wakati uliopangwa.

Kamati inaishauri wizara ya Habari vijana utamaduni na michezo kuhakikisha kuwa katika viwanja vyote vya ngumi vinatiwa vipoza hewa ili watu ambao wanaenda kuangalia michezo hiyo basi wanakuwa katika hali nzuri na salama.

Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa uwanja wa Gombani unazungushiwa uzio ili kuzuia eneo hilo kuvamiwa kwa ajili ya matumizi binafsi.

Kamati pia inaishauri Wizara kutafuta kampuni bora za kufanya usafi ili kujenga mazingira bora ya usafi katika viwanja hivyo.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kazi kubwa ya kusimamia shughuli za ujenzi wa viwanja vya Amani hadi kufikia hatua iliyofiwa.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini changamoto mbali mbali zinazolikabili Baraza la michezo la Taifa Zanzibar ikiwa pamoja na Uhaba wa fedha na wafadhili unaopelekea kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa ufanisi, Ufinyu na uchakavu wa Ofisi ya Baraza na Ukosefu wa usafiri wa kudumu wa ufuatiliaji wa kazi za kila siku za Baraza.

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kulipatia Baraza la Michezo Zanzibar nafasi katika viwanja vipya vya Amani Complex ili chombo hicho kiweze kuwa na ofisi rasmi ya kutekeleza vyema shughuli za kuendeleza sekta ya michezo kwa ufanisi.

Kamati inaupongeza Uongozi wa Wizara kwa kuhakikisha kuwa sekta ya michezo inaendelezwa pamoja na kukuza vipaji kwa vijana ili waweze kujitegemea na kujiajiri wenyewe bila ya kutegemea ajira kutoka Serikalini

Kamati inaishauri Serikali kuliongezea bajeti Baraza la Michezo la Taifa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza pamoja uendeshaji wa shughuli za Michezo kwani hivi sasa Baraza limekuwa likishindwa kutekeleza vyema majukumu yake.

Kamati inalipongeza Baraza la Michezo kwa kuunda kamati maalum ya kubuni vyanzo mbadala vya mapato ya kuendeshea shughuli za Baraza pamoja na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vya michezo yanayohusiana na utafutaji masoko katika michezo sambamba na kuendelea kuvisaidia vyama vya michezo  katika kutafuta ufadhili.

## BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto ya msingi inayoikabili Baraza hili ni Ukosefu wa Bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa Taasisi hii. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kujenga hoja kwa serikali ili taasisi hii iweze kupatiwa Bajeti na kuweza kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa mipango ya wizara husika.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Programuu hii Kamati imebaini changamoto ya Uimarishaji wa shughuli za Maendeleo ya Vijana katika kuwatafutia vijana fursa mbali mbali kwa kuwaunganisha na washirika wa Maendeleo .

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwa na mipango endelevu ya muda mfupi na mrefu ya uimarishaji wa shughuli za Maendeleo ya Vijana na kuwatafutia vijana fursa mbalimbali kwa kuwaunganisha na washirika wa Maendeleo ili waweze kunufaika na fursa hizo.

Hata hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023. Hatua hiyo itasaidia kuwa na Sera bora yenye kuainisha mahitaji na malengo ya vijana kwa mujibu wa wakati uliopo.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Programu hii, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto za Upatikanaji mdogo wa fedha za uendeshaji wa Ofisi, mrundikano makubwa wa madeni na ya muda mrefu kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar jambo ambalo linapelekea kushindwa kukamilisha kwa wakati kazi mbali mbali ambazo Wakala unatekeleza.

Vile vile Wizara kuwa na majengo chakavu na kutokuwa na nafasi ya kutosha kwa ajili ya wafanya kazi na watu wanaokuja kupata huduma, Vyama vya michezo kushindwa kujiendesha vyenyewe na hivyo kuitegemea Wizara kwa asilimia mia moja na Uhaba wa Miundombinu ya Michezo na Sanaa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya shughuli za utawala na uendeshaji kwa vyama vya michezo. Kamati inaipongeza wizara kwa kusimamia mageuzi makubwa na jitihada za kujenga miundo mbinu mipya na mizuri ya michezo.

Aidha Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023. Sambamba na Sera mpya ya Habari ya mwaka 2023 kwa kuwepo katika hatua ya kuchapishwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati viongozi wote wa Wizara zote Nne zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikanuni.

Kamati kwa upekee inazipongeza Wizara zetu ya Elimu na Afya kwa kuiwezesha Kamati kufanya ziara za kuijengea uwezo wa kujifunza mambo

mbali yanayozihusu wizara zetu kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa kweli Kamati ya Ustawi wa Jamii imeweza kujifunza mengi yanayohusu taasisi za wizara hizo na kupata uwelewa mkubwa kuhusu mafanikio na changamoto za taasisi hizo katika utekelezaji wa kazi zake na kuweza kuishauri Serikali.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi zote pamoja na wasaidizi wao kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati inapokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Kamati inampongeza Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid na uongozi wote wa Baraza pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2023/2024. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Mwisho kabisa na kwa umuhimu mkubwa Kamati inawapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusoma Muhtasari huu naomba ripoti yote iingie kwenye Hansard, Baada ya maelezo hayo ya Muhtasari wa Ripoti, naomba kutoa hoja.

Ahsante,

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**